icj International Commission of Jurists
KENYAN SECTION | Since 1959

TAARIFA MUHIMU KUHUSU HALI YA SHERIA YA HAKI YA AFYA NCHINI KENYA

Maelezo ya haki ya afya



Haki ya Afya ni haki msingi ya kibinadamu. Ni haki ya pamoja inayojumuisha huduma ya afya kwa wakati unaofaa na vigezo vya kimsingi vya kijamii vya afya, kama vile kupatikana kwa maji safi ya kunywa na usafi wa kutosha wa mazingira, usambazaji wa kutosha wa chakula salama, lishe na makazi, hali ya maeneo ya kazi na mazingira, na kupatikana kwa elimu na taarifa zinazohusiana na afya.

Haki ya uhuru na haki za afya

- √ Uhuru huu unajumuisha haki ya mtu kudhibiti afya na mwili wake (kwa mfano, uhuru wa kijinsia na uzazi) na haki ya kutoingiliwa (kwa mfano, haki ya kutoteswa, matibabu bila kibali na majaribio).

- √ Haki hizi zinajumuisha kulinda haki ya mfumo wa afya unaotoa fursa sawa kwa watu kufurahia kiwango cha juu zaidi kinachoweza kufikiwa cha afya.

Vigezo muhimu vya haki ya afya

- √ Kupatikana - vituo vya huduma ya afya, mipango na huduma za bidhaa zinafaa kupatikana kwa viwango vya kutosha ndani ya ufikiaji salama, ndani ya kilomita tano kutoka kwa idadi ya watu wanaolengwa.
- √ Kufikia - vituo vya afya na huduma zinapaswa kufikiwa kwa wote bila ubaguzi, ikiwemo ufikiaji kamili, ufikiaji wa kiuchumi, na ufikiaji wa habari.
- √ Kukubalika - vituo vya afya na huduma zinapaswa kuwa zinazofaa kitamaduni, kuzingatia jinsia, kuheshimu maadili ya kimatibabu, na usiri wa hali ya afya ya mtu binafsi.
- √ Ubora wa vituo vya afya, bidhaa, na huduma zinapaswa kuwa nzuri, za kisayansi na zinazofaa kiafya.

Mifumo ya sera na sheria kuhusu haki ya afya nchini Kenya

Katiba ya Kenya ya Mwaka wa 2010

- √ Ibara ya 43 (1)(a) inampa kila mtu haki ya kufikia kiwango cha juu zaidi cha afya, ikijumuisha haki ya kupata huduma za afya na huduma ya afya ya uzazi.
- √ Ibara ya 43(2) inaeleza kuwa mtu hafai kunyimwa matibabu ya dharura.
- √ Ibara ya 46 (1) (c) inaeleza kuwa watumiaji wana haki ya afya zao kulindwa.
- √ Ibara ya 53(1)(c) inampa kila mtoto haki ya kupata huduma ya afya.
- √ Ibara ya 56(e) inaeleza kuwa Serikali itaweka mipango ya hatua ya usawazishi ili kuhakikisha kwamba watu walio wachache na waliotengwa wanapata huduma za afya zinazofaa.
- √ Ibara ya 20 (5) inaeleza katika kutumia haki yoyote chini ya Ibara ya 43 (haki za kiuchumi na kijamii ikijumuisha haki ya afya) Serikali ikidai kwamba haina rasilimali za kutekeleza haki hiyo, ni wajibu wa Serikali kuonyesha kwamba rasilimali hizo hazipatikani. Katika ugavi wa rasilimali, Serikali itaweka kipaumbele katika kuhakikisha kufurahia zaidi iwezekanavyo wa haki au uhuru wa kimsingi kwa kuzingatia hali zilizopo, ikijumuisha udhaifu wa makundi fulani au watu binafsi.
- √ Ibara ya 21(2) inaeleza kuwa Serikali itachukua hatua za kisheria, kisera na nyinginezo, ikijumuisha kuweka viwango, ili kufikia kutimiza hatua za haki zilizoelezwa chini ya Ibara ya 43 (haki za kiuchumi na kijamii hasa haki ya afya).
- √ Ratiba ya Nne inagawa majukumu ya afya baina ya ngazi mbili za serikali. Serikali ya Kitaifa inawajibikia vituo vya afya vya kitaifa vya rufaa, sera ya afya, kujenga uwezo na usaidizi wa kiufundi kwa kaunti. Serikali za Kaunti zinawajibikia huduma za afya katika kaunti (vituo vya afya vya kaunti na maduka ya kuuza dawa; huduma za gari la wagonjwa mahututi; kuendeleza huduma ya kimsingi ya afya; kutoa leseni na udhibiti wa shughuli za kuuza chakula kwa umma; huduma za matibabu ya mifugo (ikiacha nje kudhibiti taaluma); makaburi, vyumba vya mazishi na kuchomea miili ya wafu; uondoaji wa taka, utupaji wa taka na utupaji wa taka sugu).
- √ Ibara ya 2(5) na 2(6) inaeleza matumizi ya kanuni za jumla za sheria za kimataifa na makubaliano au mkataba wowote ulioidhinishwa na Kenya kama sehemu ya sheria za Kenya. Kwa msingi huu, Kenya imefungwa na makubaliano na mkataba wa kimataifa na wa kikanda uliodhinisha na unaoeleza wajibu wa Serikali wa kuhakikisha haki ya afya.

Mifumo ya Kisheria

- √ Sheria ya Afya, 2017 imeweka mfumo mmoja wa afya ili kuratibu uhusiano kati ya Serikali ya Kitaifa na mifumo ya afya ya Serikali za Kaunti. Pia inalenga kudhibiti huduma za afya, watoaji wa huduma, bidhaa na teknolojia. Sheria hiyo inalenga kutekeleza masharti ya kikatiba yanayohusu haki ya afya.

Mfumo wa Kisheria

- √ Ruwaza ya Kenya ya 2030, chini ya nguzo ya kijamii, inalenga kuboresha mapato ya Wakenya kwa jumla kwa kutoa mfumo bora wa afya, unaolingana na wa kiwango cha juu kwa bei nafuu.
- √ Lengo la Sera ya Afya ya Kenya ya mwaka wa 2014 – 2030 ni kuhakikisha utoaji kwa wote wa huduma zinazochangia katika kutimiza haki ya afya kwa viwango vya juu zaidi vinavyoweza kufikiwa.
- √ Sera ya Huduma ya Dharura ya Kenya 2020 - 2030 inaweka mfumo wa kujumuisha huduma ya matibabu ya dharura kama sehemu muhimu ya huduma ya afya kwa wote.
- √ Sera ya Afya ya Jamii ya Kenya ya mwaka wa 2020-2030 inalenga kuwawezesha watu binafsi, familia na jamii kufikia kiwango cha juu zaidi cha afya kwa kutoa huduma za afya za jamii za ubora wa juu.
- √ Mfumo wa Mikakati wa Huduma ya Afya ya Kimsingi nchini Kenya wa mwaka wa 2019 - 2024 unatoa miongozo ya kubuni na kutekeleza mipango inayoimarisha mfumo na huduma za afya ya kimsingi nchini Kenya.

Makubaliano na Mkataba wa Kimataifa na wa Kikanda Uliodhinishwa na Kenya

- √ Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu la mwaka wa 1948 linaeleza kuwa kila mtu ana haki ya mtindo wa maisha unaotosheleza afya na ustawi, ikijumuisha chakula, mavazi, makazi, matibabu, na huduma muhimu za kijamii.
- √ Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni wa mwaka wa 1966 unaeleza kuwa Nchi Wanachama zinatambua haki ya kila mtu ya kufurahia kiwango cha juu zaidi kinachoweza kufikiwa cha afya ya kimwili na kiakili.
- √ Mkataba wa Kukomesha Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake wa mwaka wa 1979 unathibitisha ulinzi kwa wote kuhusu haki ya afya ya kutosha na unaeleza juu ya ulinzi maalumu na masuala yanayohusu wanawake.
- √ Mkataba wa Haki za Mtoto wa mwaka wa 1989 unaeleza kuwa Nchi Wanachama zitambue haki ya mtoto ya kufurahia kiwango cha juu cha afya kinachoweza kufikiwa na vifaa kwa ajili ya matibabu ya maradhi na urekebishaji wa tabia.
- √ Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa mwaka wa 2006 unaeleza kwamba Nchi Wanachama zitambue kuwa watu wenye ulemavu wana haki ya kufurahia kiwango cha juu cha afya kinachoweza kufikiwa bila ubaguzi.

- √ Lengo la tatu la Maendeleo Endelevu linaweka ajenda ya kimataifa kuhusu afya. Ajenda hiyo inalenga kuhakikisha maisha yenye afya na kuendeleza ustawi kwa umri wote kwa kupunguza mzigo wa magonjwa yaliyowekewa kipaumbele, kupunguza vifo, kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya ya ngono na uzazi na kufikia bima ya afya kwa wote.
- √ Mkataba wa Afrika wa Haki za Kibinadamu na Watu (1981) unaeleza kuwa kila mtu atakuwa na haki ya kufurahia afya bora zaidi ya kimwili na kiakili inayoweza kufikiwa.
- √ Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa mwaka wa 1990 unaeleza kuwa kila mtoto ana haki ya kufurahia hali bora zaidi ya afya ya kimwili, kiakili na kiroho.

Changamoto na Mianya Inayozuia Kufurahiwa Kamili kwa Haki ya Afya nchini Kenya

Vikwazo vya kisera na kisheria kwa utekelezaji wa haki ya afya vinajumuisha:

- √ Ukosefu wa asasi za kisheria na kisera za Kitaifa na za Kaunti za kutosha kutekeleza ipasavyo haki ya kikatiba ya huduma za afya, huduma ya afya ya uzazi na matibabu ya dharura.
- √ Ukosefu wa mikakati ya kutosha kati ya serikali ili kuhakikisha upatikanaji kwa usawa wa huduma za afya na rufaa kati ya Serikali za Kaunti na kati ya Serikali ya Kitaifa na Serikali za Kaunti.
- √ Ukosefu wa sera ya kitaifa kuhusu ruzuku ya huduma za afya unasababisha gharama kubwa za matibabu na ruzuku za huduma za afya ambazo hazilingani na gharama za utoaji wa huduma.
- √ Ukosefu wa hatua za usawa, sera na sheria za bima ya afya ya jamii ili kulinda na kuepusha makundi maskini, yaliyo hatarini na yaliyotengwa dhidi ya hatari za matumizi ya huduma ya afya.
- √ Ukosefu wa sera ya fedha za afya na miongozo ya mgao wa bajeti ya serikali kwa ajili ya utekelezaji wa haki ya kikatiba ya afya, huduma ya afya ya uzazi, matibabu ya dharura na huduma za afya.
- √ Ukosefu wa sera ya utekelezaji na usimamizi madhubuti wa huduma za afya zinazolingana, ikijumuisha utekelezaji wa haki ya kikatiba ya afya kati ya Serikali ya Kitaifa na Serikali za Kaunti.
- √ Ukosefu wa miongozo ya sera kuhusu utekelezaji wa kihatua wa haki ya afya kama ilivyoelezwa chini ya Ibara ya 21(2) ya Katiba ya Kenya na Maoni ya Jumla ya UN CESCR Na. 3 ya 1990.

Vikwazo vinavyohusiana na mfumo wa afya vya kutimiza haki ya afya vinajumuisha:

- √ Udhibiti na ufuatiliaji hafifu wa huduma za afya za kibinafsi.
- √ Ukosefu wa mkakati wazi wa kuboresha na kuendeleza programu ya majaribio ya huduma za afya kwa wote.
- √ Uhaba wa wahudumu wa kutosha wa afya katika vituo vya afya kinyume na kanuni na viwango vinavyokubalika.
- √ Ukosefu wa matumizi bora ya rasilimaliwatu iliyopo ndani ya mfumo wa afya uliogatuliwa.
- √ Mifumo hafifu ya usimamizi wa mgao wa bidhaa za matibabu, matumizi, vifaa na teknolojia ni changamoto kubwa katika kutoa huduma za afya.
- √ Ukosefu wa utambuzi rasmi na ushirikiano wa mfumo wa afya ya jamii kama sehemu muhimu ya mfumo wa afya.
- √ Ukosefu wa huduma bora za dharura za afya na rufaa katika ngazi ya kitaifa na kaunti.
- √ Usimamizi wa mfumo wa afya haukifi kiwango cha juu kwa vile baadhi ya changamoto za sekta hii zinatokana na ukosefu wa mpangilio na ushirikiano katika mfumo uliogatuliwa wa afya kati ya Serikali ya Kitaifa na Serikali za Kaunti. Mipangilio ya utawala wa kiwima kati ya ngazi mbili za serikali, yenye utaratibu mfinyu na fursa za ushirikiano kati ya serikali na uratibu katika sekta ya afya, imesalia kuwa kikwazo kikubwa cha kuhakikisha uhusiano mzuri wa kikazi na ushirikiano katika utoaji wa huduma za afya na utawala.

Mianya na changamoto za ufadhili wa kiafya unajumuisha:

- √ Hazina ya Kitaifa mara nyingi huchelewesha utoaji wa ufadhili sawa na ruzuku zenye masharti kwa Serikali za Kaunti. Fedha zinapochelewa kutolewa, Serikali za Kaunti hutatizika kufadhili shughuli zao, ikijumuisha kukidhi gharama ya kudhibiti huduma za afya kwa kuwa mgao sawa wa mapato ni sehemu ya rasilimali nyingi ambazo Serikali za Kaunti hutumia kupanga na kutekeleza majukumu yao.



- √ Ukosefu wa ugatuaji wa kutosha wa kifedha na uwajibikaji katika usimamizi wa mapato kutoka kwa vituo vya afya vya kaunti.
- √ Ukosefu wa ugatuaji wa kifedha ndani ya Serikali za Kaunti, huku mamlaka ya udhibiti ya kifedha yakiwekwa katikati ya idara za Hazina ya Kaunti ikipunguza uwezo wa idara kama vile idara ya afya na vituo vya afya wa kutoa huduma bora za afya. Pesa za afya pia hazijawekewa vidhibiti katika Serikali nyingi za Kaunti, na wakati mwingine, pesa zinazotolewa kwa ajili ya afya zinatumika vibaya au kuhamishwa kwa kazi nyingine ndani ya mifumo ya Serikali ya Kaunti.

- √ Licha ya Sheria ya Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya kusifiwa kuwa chombo kikuu cha ufadhili wa kufikia huduma ya afya kwa wote, bado haijashughulikia vya kutosha baadhi ya masuala muhimu yanayohusiana na kujumuisha jamii. Kwa mfano, maelezo ya manufaa ya afya yanayoelezwa katika kanuni hayajumuishi baadhi ya magonjwa kwa hivyo hayafaidi Wakenya walioathirika na wanaohitaji bima. Aidha, huku asilimia sabini ya Wakenya wakitafuta huduma za afya katika vituo vya afya vya umma, data kutoka Bima ya Kitaifa ya Afya (NHIF) zinaonyesha kuwa ni asilimia thelathini pekee ya malipo ya kurejeshwa yanatolewa kwa vituo vya afya vya umma. Hazina ya Kitaifa ya Afya inatoa zaidi ya asilimia sabini ya malipo kwa vituo vya afya vya kibinafsi.

Mianya na changamoto ya idadi wa wahudumu wa afya zinajumuisha

- √ Uhaba wa wafanyakazi unafanya wahudumu katika sekta ya afya ya umma kulemewa sana.
- √ Kukosa kutambua na kuwalipa wahudumu wa afya wa kujitolea katika jamii kama sehemu muhimu ya wahudumu katika mfumo wa afya ya kimsingi.
- √ Mtazamo mbaya wa baadhi ya wahudumu wa afya, uzembe, na utepetevu katika sekta ya afya ya umma.

Mianya na Changamoto ya Matibabu ya Dharura

- √ Kutokuwa tayari kwa mfumo wa afya kwa dharura za kiafya kama vile ajali na milipuko ya magonjwa.

Mianya na Changamoto za Habari za Afya

- √ Ukosefu wa sera wazi na mfumo wa kisheria wa kulinda usiri kwenye rekodi za afya na kushiriki historia ya mgonjwa katika vituo wakati wa kushughulikia kisa ni hafifu.
- √ Mfumo duni wa usimamizi wa habari za afya.
- √ Wahudumu wa kibinafsi wa afya kukosa kutoa ripoti.

Mapendekezo

Kuboresha mageuzi ya sheria, sera na mikakati itakayokuza haki ya afya

- √ Kukagua sheria za sekta ya afya na sera za umma ili kutathmini ulinganifu wao na kanuni za haki za kibinadamu, viwango, kanuni, na uwezo wa mifumo ya kitaasisi ili kuhakikisha utekelezaji wa haki ya afya kama inavyoelezwa katika Katiba ya Kenya na sheria zinazohusika.
- √ Kufafanua kwa uwazi vipengele muhimu vya haki ya afya, vikijumuisha ufikiaji, upatikanaji na ukubalifu wa ubora wa vituo vya huduma za afya, bidhaa na huduma ili kuhakikisha huduma za afya kwa wote.

- √ Kuunda sera, miongozo, na kielelezo kwa ajili ya utekelezaji wa kihatua wa haki ya afya kama inavyoelezwa katika Katiba.
- √ Kujumuisha kwa mpangilio mitazamo ya kimsingi ya jinsia na haki za kibinadamu katika kuunda sera na mikakati ya umma ya sekta ya afya ili kupunguza ukosefu wa usawa wa kijinsia na kijamii katika afya.
- √ Kutunga na kutekeleza Mswada wa Sheria ya Afya ya Uzazi wa mwaka wa 2019 ili kutoa utambuzi wa haki za uzazi na Mswada wa Sheria ya Huduma za Afya ya Jamii wa mwaka wa 2019 ili kuweka mfumo wa kudhibiti huduma za afya ya jamii ambazo ni muhimu katika kufikia huduma za afya za kinga na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya.
- √ Kukagua utendakazi sawia unaohusiana na mifumo ya habari za afya na uwekezaji unaohusika katika teknolojia na kuhakikisha mgao sawa wa fedha kati ya Serikali ya Kitaifa na Serikali za Kaunti.

Kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya

- √ Kuanzisha mkakati wa kujenga uwezo na usaidizi wa kiufundi kwa Serikali za Kaunti ili kuhakikisha usimamizi bora wa mfumo wa afya na utoaji wa huduma bora za afya.
- √ Kutekeleza Sheria ya Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya kuwa mpango wa kitaifa wa bima ya afya ya jamii ili kuhakikisha upatikanaji wa kiwango cha juu zaidi cha huduma za afya.
- √ Kujumuisha masuala ya watu wenye ulemavu katika miundo yote ya vituo vya afya, miundombinu na utoaji wa huduma.
- √ Kuimarisha uwezo wa mamlaka za udhibiti ili kuhakikisha huduma bora za afya, usalama na utendakazi wa dawa, bidhaa za afya na teknolojia.

Kuimarisha mfumo wa afya na mazingira ya kitaasisi kwa ajili ya haki ya afya ili kuboresha utoaji wa huduma

- √ Kuunda sera ya kitaifa ya utekelezaji, uratibu, hatua za pamoja na usimamizi wa huduma za afya zinazowiana.
- √ Kutekeleza Jukwaa la Mashauriano kati ya Sekta ya Afya na Serikali na taratibu nyingine za uratibu wa sekta ya afya zilizoanzishwa chini ya Sheria ya Afya ya mwaka wa 2017 kwa ajili ya kuratibu sekta ya afya katika Serikali ya Kitaifa na Serikali za Kaunti.
- √ Kuimarisha taratibu za ushirikiano wa wadau wa sekta nyingi na baina ya serikali, ushirikiano na mpangilio katika ngazi ya kitaifa na kaunti ili kushughulikia masuala ambayo yanazuia kufurahia haki ya afya.
- √ Kuanzisha Tume huru ya Huduma ya Afya ili kusimamia ipasavyo rasilimaliwatu zinazohusu afya, ikijumuisha kuajiri, kupandishwa vyeo na malipo ya wahudumu wote wa afya ndani ya mfumo wa usawa wa mipangilio ya afya ya Serikali ya Kitaifa na Serikali za Kaunti.

- √ Kuimarisha uwezo wa Serikali ya Kitaifa na Serikali za Kaunti ya kusimamia na kufuatilia haki za afya.
- √ Kuimarisha uwezo wa kijamii katika kupanga mipango shirikishi, ufuatiliaji na uwajibikaji wa kijamii kwa ajili ya ushiriki kikamilifu katika kupanga na kufuatilia haki ya afya.
- √ Kuimarisha uwezo wa mfumo wa afya ya umma ili kutoa huduma bora za afya na kuhakikisha rasilimali za kutosha zinakusanywa, kutengwa na kutumika kwa uwajibikaji, ufaafu, ufanisi, usawa, ushirikishwaji, uwazi na kwa njia endelevu.

Kuimarisha haki ya afya wakati wa dharura za kiafya na masuala ya misaada ya kibinadamu

- √ Kuunda na kutekeleza kanuni kuhusu haki ya matibabu ya dharura ili kutekeleza Sera ya Huduma ya Dharura ya Kenya ya 2020 - 2030.
- √ Kuunda miongozo ya sera ya kukabiliana na dharura za kiafya ili kujikinga dhidi ya maamuzi na vitendo vinavyohatarisha haki ya kibinadamu ya afya wakati wa kukabiliana na majanga ya kiafya.
- √ Kuunda miongozo ya sera ya kitaifa kuhusu mitazamo inayozingatia haki za kudhibiti dharura za kiafya ya umma na kulinda haki za kibinadamu na haki ya afya wakati wa dharura za kiafya kama vile milipuko ya magonjwa na majanga.
- √ Kuanzisha mkakati au mipango ya kitaifa ya kuimarisha uwezo wa mfumo wa afya kuhusu kujitayarisha na kudhibiti dharura ya kiafya ambayo inazingatia mahitaji ya makundi yaliyo katika hatari wakati wa dharura za kiafya.

Kuimarisha ufahamu na uelewa wa haki ya afya

- √ Kuanzisha mipango ya elimu kwa umma ili kuimarisha ufahamu wa haki ya afya na desturi za kijamii, kidini na kitamaduni ambazo zinazuia kupatikana kwa haki ya afya, ikijumuisha afya ya uzazi.
- √ Kuendeleza na kuunda maeneo salama kwa wananchi kushiriki vilivyo na kikamilifu katika sheria, kutunga sera, na kufanya maamuzi yanayohusiana na haki ya afya na utoaji wa huduma za afya. Juhudi hizi zinapaswa kushirikishwa na elimu ya kiraia ili kuwezesha ushirikishwaji kamili wa wananchi.
- √ Kuendeleza na kuimarisha jukumu la asasi za kiraia katika madai yenye maslahi ya umma na kuelekeza mawazo ili kuhimiza watu zaidi kufika mahakamani na kutetea kulinda haki zao hasa zinapotishiwa, kukiukwa au kukandamizwa.
- √ Kuandaa nyenzo za elimu ya habari na mawasiliano kuhusu haki ya afya na kuweka pamoja habari zinazolenga hadhira mbalimbali kama vile umma na wanaowajibika.

Ufadhili wa utoaji endelevu wa huduma za afya

- √ Kutunga sheria za fedha za afya na miongozo ya sera kuhusu mgao wa bajeti ili kutekeleza haki ya afya, huduma ya afya ya uzazi na matibabu ya dharura kwa mujibu wa Katiba.
- √ Kuongeza mgao wa bajeti kwa afya na serikali za kitaifa na kaunti ili kutimza dhamira ya azimio la Abuja ya kutenga angalau asilimia 15 ya Pato la Taifa kwa sekta ya afya ifikapo mwaka wa 2030 kupitia kuboresha bajeti katika miaka ya fedha inayofuata. Hiyo ni kwa ajili ya kuharakisha upatikanaji wa huduma za afya ili kufikia Bima ya Afya kwa wote.
- √ Kuainisha gharima kamilifu ya utekelezaji wa haki ya kikatiba ya huduma za afya, huduma ya afya ya uzazi na matibabu ya dharura na majukumu ya afya chini ya Ratiba ya Nne kwa mujibu wa Ibara ya 187(2) ya Katiba kuhusu kanuni ya rasilimali ambayo lazima ifuate na kuwiana na majukumu.
- √ Kuanzisha ufadhili wa huduma za afya za Kaunti kupitia kuwezesha sheria za Kaunti kulinda mapato ya ndani yanayotokana na vyanzo mbalimbali na fedha zilizoidhinishwa na Mabunge ya Kaunti.
- √ Kuimarisha mpangilio wa wafadhili kwa ajili ya uwekezaji unaofaa na wenye ufanisi katika kutekeleza haki ya afya kwenye ngazi zote za serikali na asasi za kiraia.
- √ Kuendeleza mazungumzo ya kimkakati na sekta binafsi kuhusu ufadhili wa afya, kwa kuzingatia wajibu wa Serikali chini ya Tume ya Afrika ya Haki za Kibinadamu na Haki za Watu kusimamia kikamilifu utoaji wowote wa kibinafsi wa huduma za kijamii ili kuhakikisha kuwa wahusika hao wanaweka kipaumbele kwenye maslahi ya umma badala ya maslahi ya kibiashara.
- √ Kuhakikisha utekelezaji wa Mkakati wa Ufadhili wa Afya wa Kenya wa mwaka wa 2020-2030 na ufadhili wake katika ngazi ya Kaunti ili kuboresha matumizi ya fedha za umma katika afya. Hii itasaidia kuhalalisha matumizi ya afya, kuboresha ufanisi wa misaada na kuhakikisha utoaji wa mikakati ya kutosha ya usalama kwa watu maskini na walio hatarini nchi kuelekea kufikia bima ya afya kwa wote na haki ya Kikatiba ya afya..

Imechapishwa na:

icj International Commission of Jurists
KENYAN SECTION | Since 1959

Bewa la Kenya la Tume ya Kimataifa ya Wanasheria (ICJ Kenya)
Jumba la ICJ Kenya, Kwenye barabara ya Silanga, Karen,
S.L.P 59743 – 00200, Nairobi, Kenya
Baruapepe: info@icj-kenya.org
Tovuti: https://icj-kenya.org
Facebook: @ICJ.Kenya
Twitter: @ICJKenya

Imefadhiliwa na

ROYAL DANISH EMBASSY
Danida

Uraia
Kenya's National Civic Education Programme